JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**
ISO 9001:2015 CERTIFIED

**KATIKA KAMATI YA MAUDHUI YA MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA, DAR ES SALAAM**

**SHAURI NA. 09 - 2020/2021**

**DHIDI YA**

**RADIO ONE STERIO**

# UAMUZI

**UAMUZI WA KAMATI YA MAUDHUI KUHUSU TUHUMA ZA UKIUKAJI WA KANUNI ZA MAWASILIANO YA KIELEKTRONIKI NA POSTA (MAUDHUI YA UTANGAZAJI WA REDIO NA TELEVISHENI), 2018.**

## 1.0 MAELEZO KUHUSU UKIUKAJI WA KANUNI

1.1 Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ilitoa leseni ya kurusha Matangazo (Matangazo ya Redio) kwa Kituo cha Utangazaji cha **Radio One Sterio** kwa ajili ya kutoa huduma ya utangazaji wa maudhui kwa njia ya redio.

1.2 Tarehe 29 Julai, 2020 kati ya Saa 12.00 na Saa 12.30 asubuhi, Kituo cha **Radio One Sterio** kinatuhumiwa kukiuka Kanuni na Maadili ya Utangazaji kupitia kipindi cha ***Amka na BBC***, kwa kurusha maudhui bila kuzingatia mizania ya habari pale walipokuwa wakimhoji Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Bw. Tundu Lissu, juu ya viongozi wa chama hicho kutoshiriki katika kutoa heshima za mwisho kwa aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tatu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Benjamin William Mkapa.

1.3 Mtangazaji wa kipindi hicho wakati akimhoji Bw. Tundu Lissu aliruhusu kurushwa kwa habari iliyoegemea upande mmoja pale Bwana Tundu Lissu alipotoa tuhuma na kulalamika kuwa Serikali ilimnyima nafasi ya kutoa heshima za mwisho kwa Hayati Benjamin William Mkapa, bila kumtafuta Msemaji wa Serikali ili aweze kutolea ufafanuzi tuhuma hizo, jambo ambalo ni kinyume na Sheria, Kanuni na Maadili ya Uandishi na Utangazaji wa Habari.

1.4 Wakati wa kipindi cha ***Amka na BBC***, Bw. Tundu Lissu alisikika, pamoja na maneno mengine, akizungumza yafuatayo:

***"...Inasikitisha sana, tumefika kwa wakati tulioambiwa kwa mujibu wa ratiba. Kutuambia kwamba hatuwezi kuingia uwanjani kwa sababu tumechelewa tuliona ilikuwa ni namna tu ya kusema kwamba hawataki tushiriki kumuaga huyu aliyekuwa Rais wetu...Haiwezekani tena kama hutakiwi na waandaaji wa msiba ukilazimisha kwenda watakwambia wewe ndo mchawi. Sisi hatutaki kuonekana ni wachawi wa mzee Mkapa, tumesema waendelee tu Mungu awabariki.".***

## 2.0 KANUNI ZILIZOKIUKWA

Kitendo cha **Radio One Sterio** kurusha kipindi kilichoituhumu Serikali bila ya kuthibitisha ukweli wa madai yaliyotolewa katika taarifa hiyo kutoka kwenye vyanzo husika na kwa kutozingatia mizania, **Radio One Sterio** wanatuhumiwa kukiuka Kanuni Na.15(2) (b) na (c) na 16 za Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni) 2018 ambazo zinasomeka kama ifuatavyo:

*15. (2) The licensee shall-*
*(b) report accurately, impartially, fairly and in a non- partisan manner;*
*(c) report news in an objective and balanced manner, without intentional or negligent departure from the facts, whether by distortion, exaggeration, misrepresentation or material omission.*

*16. A content service licensee shall ensure that, during the presentation of current affairs programme, factual programmes and documentaries; where issues of public importance are discussed, reasonable effort is made and reasonable opportunity is given to present a fair, accurate, balanced and impartial view.*

## 3.0 WITO WA KUTOA MAELEZO YA UTETEZI

Tarehe 05 Agosti, 2020, Kamati ya Maudhui iliuandikia uongozi wa **Radio One Sterio** wito wa kuwasilisha utetezi wao wa maandishi pamoja na kufika mbele ya Kamati ya Maudhui kujieleza dhidi ya tuhuma zinazowakabili.

Tarehe 10 Agosti, 2020, Uongozi wa **Radio One Sterio** uliwasilisha utetezi wa maandishi uliosainiwa na **Joyce Mhaville**, Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo. Pia, tarehe hiyo hiyo, Uongozi huo ukiwakilishwa na **Deogratius Rweyunga** na **Xavier Maleko** ulifika mbele ya Kamati kutoa utetezi.

## 4.0 KUSOMEWA SHITAKA NA KUSIKILIZA MAUDHUI YA RADIO ONE STERIO

Kamati ya Maudhui iliusomea Uongozi wa **Radio One Sterio** shitaka lao. Pia, Kamati ya Maudhui na Uongozi wa **Radio One Sterio** walisikiliza maudhui yaliyotangazwa na **Radio One Sterio** katika tarehe tajwa hapo juu na kisha kuualika Uongozi huo kujitetea ili kujiridhisha iwapo maudhui hayo yalikiuka Kanuni au la.

## 5.0 UTETEZI WA RADIO ONE STERIO

Katika maelezo yao ya maandishi**, Radio One Sterio** walisema kuwa wana mkataba na Kituo cha Utangazaji cha **BBC** kwa ajili ya kurusha matangazo yake ya **Amka na BBC** kila siku Saa 12.00 hadi Saa 12:30 asubuhi pamoja na kipindi cha **Dira ya Dunia** kila siku za Jumatatu hadi Ijumaa, Saa 12:30 jioni hadi Saa 1:30 usiku. Walieleza kuwa katika mkataba huo, **Radio One Sterio** wanatakiwa kupokea na kurusha matangazo ya Kituo cha **BBC** ambayo wameandaa wao BBC kuanzia utayarishaji hadi urushwaji wa vipindi hivyo hewani.

Waliendelea kusema kuwa uwepo wa Kituo cha **BBC** hapa nchini upo kisheria kwa kufuata mlolongo wote wa usajili na Kanuni za Utangazaji zinazosimamiwa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) na kwamba ushirikiano baina ya **Radio One Sterio** na **BBC** upo kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za nchi.

Walidai kwamba katika kipindi hicho cha **Amka na BBC**, hakuna sehemu yo yote ambayo **Radio One Sterio** wamehusika kwa namna yo yote katika utayarishaji wake au katika mahojiano na Bw. Tundu Lissu kwani hicho kipindi kinamilikiwa na **BBC**. Walidai kwamba wanasikitika kuona **Radio One Sterio** wanataka kuadhibiwa kwa kosa ambalo halihusiki na Kituo chao bali limefanywa na **BBC** ambacho pia kimepewa leseni ya kufanya kazi hapa nchini na Mamlaka mbali mbali za Serikali ikiwemo TCRA. Waliendelea kudai kwa kuwa **BBC** wanafahamu Sheria na Kanuni za Utangazaji za hapa nchini, shitaka hili linapaswa kuelekezwa moja kwa moja kwa **BBC** kwa kuwa ndiyo waliofanya mahojiano na Bw. Tundu Lissu.

Walimaliza kwa kuiomba Kamati isiwachukulie hatua zo zote kwa sababu hawajawahi kuitwa hata siku moja mbele ya Kamati tangu kuanzishwa kwa **Radio One Sterio** mwaka 1994 na kwamba wamekuwa wakilinda heshima na maudhui yao siku zote, jambo ambalo limekifanya Kituo chao kuheshimika na kuaminika mbele ya jamii, Serikali na Taasisi mbali mbali kutokana na Weledi mkubwa walionao.

Pia, **Radio One Sterio** ilitoa utetezi wao wa mdomo kama ifuatavyo:

**Deogratius Rweyunga,** wakati akiulizwa maswali na Kamati alisema kuwa sio kwamba kila wanacholetewa na **BBC** wanakirusha na mara kadhaa wamekuwa wakikata hewani matangazo ya **BBC** yasiyofaa. Pia, alisema kuwa vipindi vya **BBC** vya kurekodiwa huwa wanavipitisha katika mchakato mrefu kabla ya kuvirusha ili kuhakikisha kuwa havikiuki Sheria lakini hiki kinachotuhumiwa kilikuwa mubashara. Alieleza kuwa wanasikitika kwa maana walidhani **BBC** wangemuhoji Msemaji wa Serikali baada ya tuhuma za Tundu Lissu lakini hawakufanya hivyo. Alidai wao, **Radio One Sterio** katika kipindi chao cha Nipashe, kilichofuata baada ya kipindi cha **Amka na BBC**, walitangaza alichosema Msemaji wa Serikali kuhusu utaratibu wa msiba ili kurekebisha tatizo lililotokea. Alisema hawezi kuuongelea sana mkataba wao na **BBC** kwa maana hajausoma kwa karibu.

Alimaliza kwa kushukuru kuwa kikao kimekuwa cha kuwajenga, hivyo wanachukua ushauri wote wa Kamati na kwenda kuufanyia kazi haraka sana kwani Tanzania ni yetu na wana wajibu wa kuhakikisha Sheria na Kanuni zinafuatwa katika kazi zao. Aliahidi kuwa watakuwa makini zaidi kwani hii ni mara yao ya kwanza kuitwa na Kamati na katika kipindi hiki cha Uchaguzi Mkuu, watajitahidi sana kuwa makini.

## 6.0 TATHMINI YA KAMATI

6.1 Kamati ya Maudhui imebaini kwamba **Radio One Sterio** imetenda kwa uzembe kosa la kutangaza maudhui bila ya kuzingatia mizania ya habari kwa kushindwa kwao kufanya juhudi zo zote za kumtafuta Msemaji wa Serikali ili kutolea ufafanuzi tuhuma dhidi ya Serikali walizoruhusu zirushwe hewani kupitia chombo chao. Sheria, Kanuni na maadili ya fani zinawataka kutoa fursa kwa Msemaji wa Serikali kutolea ufafanuzi tuhuma hizo katika kipindi kile kile walichotolea tuhuma;

6.2 Kamati ya Maudhui imebaini kwamba utetezi wa **Radio One Sterio** kuwa wamiliki wa maudhui yanayotuhumiwa ni **BBC** hauna mashiko yo yote kwa sababu **Radio One Sterio** ndio wanamiliki leseni ya Utangazaji wa Habari hapa nchini, hivyo **Radio One Sterio** wana wajibu wa kuhakikisha kuwa maudhui yote wanayotangaza, yaliyozalishwa hapa nchini au wanayopokea kutoka vyombo vya habari vya nje ya nchi, yanazingatia weledi. Maudhui yanapaswa kufuata Sheria, Kanuni na Maadili ya Uandishi na Utangazaji wa Habari, masharti ya leseni yao pamoja na Utamaduni wa Mtanzania;

6.3 Kamati ya Maudhui imebaini kuwa **Radio One Sterio** wana Usimamizi dhaifu wa vipindi vyao hasa wanavyopokea na kuvirusha kutoka vyombo vya habari vya nje ya nchi, jambo lililosababisha wao kutangaza habari isiyokidhi matakwa ya kisheria na Kimaadili.

6.4 Kamati imeona kuwa mkataba walioingia **Radio One Sterio** na **BBC** wa kuwataka **Radio One Sterio** kutangaza maudhui wanayopokea kutoka **BBC** kama yalivyo, una upungufu mkubwa kwa sababu unaweza kuwapelekea **Radio One Sterio** kutangaza maudhui yanayokiuka Sheria na Kanuni zinazosimamia chombo chao kama ilivyotokea katika kosa hili;

4.1 Hivyo, Kamati ya Maudhui imeridhika kuwa **Radio One Sterio** imetenda kosa la kurusha kipindi kilichoituhumu Serikali bila ya kuthibitisha ukweli wa madai yaliyotolewa katika taarifa hiyo kutoka kwenye vyanzo husika na kutozingatia mizania ya Uandishi na Utangazaji wa Habari, kinyume na Kanuni Na. 15(2) (b) na (c) na Na. 16 za Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni) 2018.

## 5.0 USHAURI WA KAMATI KWA RADIO ONE STERIO

Kutokana na makosa yaliyobainika, Kamati inaushauri Uongozi wa **Radio One Sterio** kuimarisha Usimamizi wa maudhui yao ili kuepuka utangazaji wa maudhui yasiyozingatia weledi, yasiyokiuka Sheria,

Pia, **Radio One Sterio** wanashauriwa kupitia upya mikataba yao na vyombo vya utangazaji wa habari vya nje ya nchi ili kuhakikisha masharti ya mikataba yao yanazingatia Sheria, Kanuni na Maadili ya Uandishi na Utangazaji wa Habari pamoja na masharti ya leseni yao na Utamaduni wa Mtanzania.

## 6.0 UAMUZI WA KAMATI

Baada ya kuutafakari kwa kina utetezi uliotolewa na Uongozi wa **Radio One Sterio**, Kamati ya Maudhui imeridhika pasi na shaka kuwa **Radio One Sterio** wamekiuka Kanuni tajwa za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni), 2018.

Hivyo basi, Kamati ya Maudhui inatoa adhabu zifuatazo kwa **Radio One Sterio:**

1. Wanapewa Onyo Kali;

2. Wanawekwa chini ya uangalizi kwa muda wa miezi mitatu (3) pamoja na kutahadharishwa kuwa hatua kali zaidi za kisheria zinaweza kuchukuliwa dhidi yao iwapo hawatajirekebisha na kurudia makosa kama hayo ndani ya muda tajwa.

Uamuzi huu umetolewa Dar es Salaam, leo tarehe **14 Agosti, 2020**.

Haki ya kukata rufaa dhidi ya uamuzi huu kwenye Baraza la Ushindani wa Haki Kibiashara (Fair Competition Tribunal – FCT) iko wazi ndani ya siku 21 (ishirini na moja) kuanzia siku ya kutolewa kwa uamuzi huu.

**Uamuzi huu umesainiwa na:**

**Joseph Method Mapunda**

MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA
S. L. P. 474
DAR ES SALAAM
TANZANIA

.................................................................

**Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Maudhui**

**PAMOJA NA WAJUMBE WAFUATAO WA KAMATI YA MAUDHUI:**

1. **Abdul Ramadhani Ngarawa**.......................................
2. **Derek Kaitira Murusuri**.......................................
3. **Jacob Gregory Tesha**.......................................